# Karibu na Maria

*Pamoja na Leo XVI, tumtafakari Maria katika* ***Kupalizwa kwake Mbinguni*** *(Agosti 15) na tumkabidhi nia zake, ambazo pia ni zetu na zile za ulimwengu unaoteseka.*



« TUMKABIDHI MARIA
Huduma ya Askofu wa Roma, mchungaji wa Kanisa zima,
**Tunageuka…kuelekea Nyota ya bahari,** Mama wa Shauri Jema, **kama vile kuelekea alama ya matumaini**.
Tunaomba kwa maombezi yake zawadi ya **amani, msaada** na **faraja** kwa ajili ya wale wanaoteseka,
neema kwa ajili yetu sisi sote **ya kuwa mashahidi** wa Bwana Mfufuka.
**Maria Mtakatifu sana**, Mwanamke wa Pentekoste, **Bikira aliyetembelewa na Roho Mtakatifu,** Mama aliyejaa neema, atusindikize na atuombee.
Tujikabidhi sote kwa maombezi ya Maria Mtakatifu Sana.
Kwa kazi ya Roho Mtakatifu, amekuwa ***"Makao Matakatifu ya Mungu"***.
¨pamoja naye, tunaweza pia kufanya uzoefu wa furaha ya kumkaribisha Bwana na kuwa alama na chombo cha upendo wake.
Maria Mama wa Mungu atusaidie kutembea pamoja katika njia ya amani. »
***Maria Mtakatifu, Mama wa Mungu, utuombee.***

## Julai 8 Sikukuu ya Mwenyeheri Petro Vigne

*Tarehe 8 Julai Kanisa linaadhimisha sikukuu ya Mwenyeheri Petro Vigne, Padre mmisionari na mwanzilishi… Linafanya hivyo, na sisi sote tunafanya hivyo pia, tukitoa shukrani kwa Mungu :* ***kwa mfano aliotoa unatutia moyo, kwa mafundisho yake unatuangazia, kwa sala zake unatulinda. ».***

*>>> tunamkabidhi Mkutano Mkuu wa Shirika ambao utafanyika kuanzia 11 hadi 26 Julai, huko Valence.*

**MWEZI WA AGOSTI** pia ni mwezi « wa kuzingatia » ufahamu wetu wa Mwenyeheri Petro Vigne. Mnaweza :

- Kuadhimisha kumbukumbu yake ya kuzaliwa : tarehe 20 Agosti 1670, huko Privas., na kumbukumbu yake ya Ubatizo : tarehe 24 Agosti …kwa yeye, siku maalum muhimu, kwa sababu : *ni siku ambapo tumeitwa kwa ajili ya Injili,* ni ufufuko wa pekee", alisema… ! anatuita pia kukumbuka Ubatizo wetu !


**WATAWA WA SAKRAMENTI TAKATIFU**
NYUMBA MAMA: 113, AVENUE VICTOR HUGO 26000 VALENCE - UFARANSA



N° 07-08. 2025
*Imetolewa : Shirika la Masista wa Sakramenti Takatifu*


# NENO Mwenyeheri PETRO VIGNE Leo

Tarehe 8 Mei *2025 tulimkaribisha kwa furaha Papa wetu Leo XIV. Anatoka Peru, alizaliwa Marekani, mtawa Mwagustino. Tulisindikiza kwa hisia ujumbe wake wa kwanza kabisa. Tunapaswa kumsindikiza katika utume huu mzito alionao sasa. Roho Mtakatifu amwongoze, na Bikira Maria amsindikize.*

## FURAHA na Papa wetu Leo XIV

*Amani iwe nanyi nyote !...* hii ni salamu ya kwanza ya Kristo Mfufuka, Mchungaji Mwema aliyetoa maisha yake kwa ajili ya kundi la Mungu.
Nami pia, **ningependa salamu hii ya amani iingie ndani ya mioyo yenu, iwafikie familia zenu,** watu wote, popote walipo, **watu wote, dunia nzima**.
Ni amani ya Kristo Mfufuka, amani inayovua na kupokonya silaha, nyenyekevu, na stahimilivu. Inatoka kwa Mungu. Mungu ambaye anatupenda sisi sote bila masharti. *Mei 8*

Nalichaguliwa bila sifa yoyote na, kwa hofu na kutetemeka,
***nakuja kwenu kama kaka anayetaka kuwa mtumishi wa imani yenu na wa furaha yenu ,*** nikitembea pamoja nanyi katika njia ya upendo wa Mungu, unaotaka sisi sote tuungane katika familia moja



Katika familia, **imani inarithishwa na maisha,** kutoka kizazi hadi kizazi : inashirikishwa kama chakula kwenye meza na mivuto ya moyo. Hii inafanya kuwa **mahali pa pekee pa kukutana na Yesu,** anayetupenda na anataka mema yetu daima. *1st Juni*

kutupa nyavu tena na tena ili **kuzamisha katika maji ya ulimwengu tumaini la Injili,** wasafiri juu ya bahari ya maisha ili wote waweze kujikuta katika kumbatio la Mungu. *Mei 18*

Kwa miezi hii ya Julai na Agosti Papa wetu Leo pia anatuachia jumbe ambazo zinaweza kutusindikiza na kututia moyo. Maisha yetu yanaweza « kuzidisha matumaini » kando kando yetu

# Kuzidisha matumaini

**Kwa nguvu ya Roho Mtakatifu… enendeni na pelekeni kwa kila mtu tumain la Bwana Yesu**. *Juni 8*



**Mungu hupanda mbegu ya neno lake juu ya kila udongo,** yaani **katika hali zetu zozote :** wakati mwingine sisi ni wa juu juu na wa kukengeushwa**,** wakati mwingine tunajiachia kuchukuliwa na furaha wakati mwingine tunalemewa na wasiwasi wa maisha, lakini pia kuna nyakati ambapo tunajionyesha wapatikanaji na wakaribishaji.

**Mungu anaamini na anatumaini** kwamba kwa kuwahi au kwa kuchelewa mbegu hiyo itachanua. Anatupenda hivi : **hatungoji tuwe udongo mzuri**, daima anatupa neno lake kwa ukarimu. **Pengine kwa kuona kwamba anatuamini, tamaa ya kuwa udongo mzuri itazaliwa ndani yetu.**

**HAYA NDIYO MATUMAINI,** yaliyojengwa juu ya mwamba wa ukarimu na wa huruma ya Mungu. *Mei 21*

**Tunataka kuuambia ulimwengu, kwa unyenyekevu na kwa furaha : mtazameni Christo ! mkaribieni Yeye !Lipokeeni Neno lake linalotia nuru na kufariji!** Sikilizeni pendekezo lake la upendo la kuwa familia yake pekee.

*"…Unapokuwa thabiti kuamini kwa unyenyekevu kwa Mchungaji wa kwanza, umeunganishwa, si kwenye matawi madogo ya mti, bali ya mti mkubwa. Kwa hivyo huogopi mabadiliko ya maoni ya wanadamu.*



*Zaidi ya hayo,* ***mshiriki aliyeunganishwa kwa uthabiti na kichwa kinachoonekana cha Kanisa anapokea roho ya kichwa kisichoonekana kinachomwongoza:*** *Yesu Kristo, wakati imani yake, nyenyekevu, tii na hai inapomfanya ashikamane naye kwa uthabiti."*

**Rt de Vie.1. 219**

*Kuwa na likizo au la…Katika hili « **Neno…kwa leo** » Petro Vigne anakualika kujipa burudani kidogo, hakika ni rahisi sana. Labda hii itakuwa namna yako ya « kuzidisha matumaini » ndani yako na karibu na wale walio pamoja na wewe…**Achia upinde**…ili usirushe mishale, kwa maneno, kwa sura, kwa ishara. Utajisikia vizuri na Mtakatifu Paulo, pamoja na Petro Vigne watanong'ona katika sikio lako : Furahi !*

# Kuweza kupumzika

*"Furahini katika Bwana wetu, asema Mtume Paulo, nasema tena : furahini ; wema wenu na ujulikane na wote, kwa maana Bwana yu karibu ". Fl.4 :5*

***Furahini…***

*Cassian anasimilia kwamba Mt.Yohane Mwinjili alikuwa akijivinjari na kware : hii ilikuwa imewakashfu wawindaji !*



*Mtume huyu Mkubwa alimfanya aelewe kwamba, kama vile upinde wake wakati mwingine unapaswa kuachiliwa,* ***roho ya mwanadamu ni lazima pia iweze kupumzika*** *katika shughuli zake za kiroho…*

*Mtakatifu Louis alitaka kwamba baada ya mlo yasemwe* ***maneno machache ili kufurahisha…***

*Huyu anasema, mazungumzo mabaya yasitoke vinywani mwenu. Na yatoke mazungumzo mazuri tu yenye uwezo wa kulisha imani, ili itie mvuto wa utakatifu kwa wale wanaowasikiliza…*

*Uchungu, ghadhabu, hasira, kelele na matukano, hayo yote lazima yatoweke kati yenu, anasema tena Mtakatifu Paulo (Efe. 4 :31). Pia hupaswi kamwe kuonekana kitoto katika maneno na matendo yako !...*

*Ni lazima kudumisha hali ya furaha katika mapumziko au tafrija, kati ya maneno yanayosemwa kwa ajili ya kuburudisha na yale yanayosemwa kwa ajili ya kujenga !*

*Kwa kufanya hivyo, kwa namna ambayo* ***wokovu wa roho na afya ya mwili vyote viwili vinapata manufaa yao.***

**H.N.II-85-86.**

Vigne M.E.P. missionnaire